# Standard 5 End Term 1 Exam, 2016

## KISWAHILI

MUDA: SAA 1 DAK. 40

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1-15, kwa kutumia jibu bora**

Wawindaji haramu wanaharibu uchumi ____1____ nchi yetu. Wao ____2____ wanyama wa pori. Wanyama ____3____ wanaletea nchi yetu pesa nyingi ____4____ huja nchini ____5____ kuwaona wanyama hawa.
Siku ____6____ wawindaji hawa walikuwa ____7____ kazi yao haramu. ____8____ walikuwa msituni ____9____ wawindaji hawa ____10____ mbali walioacha watu. Walipofika ____11____ nao waliona kuwa walikuwa majangili. ____12____ wameangamiza ndovu ____13____ waliwashika na ____14____ silaha zao ____15____.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. ya | B. wa | C. la | D. za |
| 2. | A. wanauwa | B. wanawauwa | C. wanaua | D. wanawaua |
| 3. | hizi | B. huyu | C. hawa | D. haya |
| 4. | A. wakimbizi | B. watalii | C. watoro | D. walowezi |
| 5. | A. mwetu | B. yetu | C. letu | D. muetu |
| 6. | A. moja | B. mumuja | C. mmoja | D. monja |
| 7. | A. kwa | B. na | C. katika | D. kwenye |
| 8. | A. Maaskari | B. Mapolisi | C. Polisi | D. Askari |
| 9. | A. waliwaficha | B. wakiwatafuta | C. wakiwalinda | D. wakiwasumbua |
| 10. | A. Kwa | B. Na | C. Pa | D. Mwa |
| 11. | A. mbali | B. kando | C. nyuma | D. karibu |
| 12. | A. walikua | B. hawakua | C. walikuwa | D. hawakuwa |
| 13. | A. mawili | B. mbili | C. miwili | D. wawili |
| 14. | A. kuwa nyaganya | B. kuwanyang'anya | C. kuwapa | D. kutupa |
| 15. | A. sote | B. zote | C. yote | D. lote |

**Kutoka swali la 16-30, chagua jibu sahihi kulingana na maagizo**

16. Unataka nguo yako ishonwe ________?
A. vipi B. upi C. nani D. ipi

17. Wageni walipotembea kwetu, niliwawekea maji kwenye ______________
A. birika B. bilauri C. mbuzi D. uteo

18. Wakati wa kiangazi mimea _______ maji.
A. hupaliliwa B. hupigwa
C. hufyekwa D. hunyunyiziwa

19. Umbo hili ni gani?



A. sambamba
B. tufe
C. wimbi
D. zigizagi

20. Ugonjwa unaomfanya mtu kuanguka na kupoteza fahamu huitwa
A. Kifafa B. Ukimwi C. Kichocho D. Kifaduo

21. Neno **kufuli** liko katika ngeli gani?
A. A - WA B. I - ZI
C. LI - YA D. YA - YA

22. Ni jina lipi halifai kati ya haya?
A. Ninga B. Kipanga
C. Sigi D. Swara

23. Kitambaa cha kufunika dirisha huitwa______
A. zulia B. foronya
C. busati D. pazia

24. Rangi ambayo huonyesha maji ni ______
A. manjano B. urujuani
C. zambarau D. samawati

25. **Kamilisha methali:** Dawa ya moto ni __________
A. maji B. wazima moto
C. moto D. mvua

26. **Kitendawili**
Babu, mama na watoto mnaenda wapi?
A. Siafu B. Ng'ombe
C. Wasafiri D. Wadudu

27. 1, 969 kwa maneno ni ________
A. Elfu moja mia sita tisini na sita
B. Elfu moja mia tisa sitini na sita
C. Elfu moja mia tisa sitini na tisa
D. Elfu moja mia sita tisini na tisa

28. Mama ya shangazi yangu ni _________
A. hale B. nyanya C. mbiomba D. mjukuu

29. Jibu la _______ ni marahaba.
A. habari B. uhaligani
C. shikamoo D. alamsiki

30. Chagua sentensi sahihi
A. Juma alilewa na nyanya
B. Nilimsikilia huruma sana
C. Kitabu hiki ni safi
D. Kaka ni mchezaji mhodari

**Soma habari hii kisha ujibu maswali 31-40**

Siku moja Josto alipokuwa akitoka shuleni alishikwa na kikohozi. Usiku huo alikohoa sana. Keshoye mama yake alimpeleka hospitlaini.

Daktari alimkagua na kumpa dawa iliyokuwa katika chupa. Daktari alimwambia Josto awe akitikisa chupa kabla ya kunywa dawa.

Baada ya siku mbili, Josto alikunywa dawa hiyo bila kutikisa chupa. Mara tu alipokumbuka masharti ya daktari alimwita dada yake. Alimwamuru dada yake amtikise kama chupa ya dawa.

Mama yake aliingia na akauliza kwa nini Josto alikuwa akitikiswa. Josto alimjibu kuwa ni kwa sababu aliinywa dawa bila kutikisa chupa, ndipo akaamua atikiswe ili dawa ichanganyika tumboni.

Mama yake alimwambia kuwa ni hatari kusahau masharti ya daktari kwa sababu kunaweza kusababisha madhara makubwa zaidi.

31. Josto aliugua nini?
A. Kikohozi B. Kuendesha
C. Vidonda D. Kukatwa

32. Josto alitibiwaje na daktari?
A. Kudungwa sindano
B. Alipewa tembe
C. Apewa chupa
D. Alipewa dawa maji maji

33. Josto alisahau kufanya nini?
A. Kunywa dawa
B. Kutikiswa baada ya kunywa dawa
C. Kutikisa chupa baada ya kunywa dawa
D. Kutikisa chupa kabla ya kunywa dawa

34. Dada yake Josto aliamua kufanya nini?
A. Kuitikisa chupa B. Kumtikisa Josto
C. Kuitikisa dawa D. Kumtikisa mama

35. Josto alikuwa akitoka wapi alipougua?
A. Shuleni B. Sokoni
C. Hospitalini D. Kucheza

36. Kusahau masharti ya daktari kunaweza kusababisha______
A. faida B. furaha
C. madhara D. mapenzi

37. Jina jingine la daktari ni _________
A. nahodha B. tatibu C. rubani D. mhadhiri

38. Mama alipoingia chumbani alikuta
A. Josto akinywa dawa
B. Josto akimtikisa dada yake
C. Josto akitikiswa
D. Josto akitetemeka

39. Josto alikuwa ___________
A. mpole B. mcheshi C. mwerevu D. mjinga

40. Taarifa hii inatufundisha
A. tusifuate maagizo
B. tusingatie masharti tunayopewa
C. tuwe wahaha ulifu
D. tupuuze masharti tunayotolewa

**Soma habari hii kisha ujibu maswali 41-50**

Shule ya Msingi ya Bidii,
Sanduku la Posta 334,
Kibao.
15-09-2016

**Kwa rafiki Kela,**

Natoa salamu nyingi sana kutoka kwetu hapa mjini. Wewe hujambo hapo ulipo? Je, masomo yaendeleaje?

Hapa tunafanya bidii sana katika masomo yetu. Dada anajitayarisha kwa mtihani wake wa darasa la nane. Mimi na dada yangu tunasoma sana ili tusishindwe na wenzetu darasani. Mwisho wa muhula uliopita nilishikilia nafasi ya tatu. Baba, mama na wajomba wote walifurahi sana. Walinipa zawadi.

Wasalimie wazazi, ndugu na marafiki zako. Tafadhali niandikie barua upatapo waraka huu.

Ni rafiki yako,
**Kuto Opeto.**

41. Barua hii iliandikwa na nani?
A. Kola B. Mzazi C. Opeto D. Dada

42. Unafikiri kuwa barua hii iliandikwa muhula gani?
A. Wa pili B. Wa tatu
C. Wa kwanza D. Septemba

43. Kulingana na taarida mwandishi
A. anafanya bidii B. ni mzembe
C. anaburura mkia D. ni mjinga

44. Mwandishi alikuwa nambari tatu mwisho wa muhula wa ___________
A. kwanza B. pili C. tatu D. mwaka

45. Jina jingine la barua kulingana na taarifa hii ni
A. anuani B. muhula C. bidii D. waraka

46. Jina la mji ulioko karibu sana na mwandishi ni
A. Kibao B. Kola C. Kutu D. Opeto

47. Nani anayejitayarisha kufanya mtihani wa darasa la nane?
A. Kola B. Dada Kuto
C. Dadaye Kola D. Kato

48. Kola alipewa zawadi na nani __________?
A. Baba, mama, shangazi
B. Mama, shangazi, wajomba
C. shangazi, mama, mjomba
D. wajomba, mama, baba

49. Jibu la hujambo ni __________
A. marahaba B. sijambo
C. hatujambo D. mzuri

50. Taarifa hii ni mfano wa
A. hotuba B. barua rasmi
C. shairi D. barua ya kirafiki